# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

# SKULI YA SHERIA ZANZIBAR

Skuli ya Sheria Zanzibar ilianzishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sheria namba 13 ya mwaka 2019. Kupitia sheria hii, Skuli ya Sheria pamoja na mambo mengine imepewa mamlaka ya kuwafunza watu wapate kuwa Mawakili au Vakili wenye sifa.

Kwa mamlaka iliyopewa Skuli ya Sheria Zanzibar chini ya kifungu namba 7 (2) (h) cha Sheria iliyoanzisha Skuli. Kwa mamlaka hayo, Skuli ya Sheria Zanzibar inatangaza nafasi za kazi katika maeneo yaliyoainishwa hapo chini, kwa Wazanzibari wenye sifa zinazohitajika:

1. **AFISA UDHIBITI UBORA DARAJA LA II (QUALITY ASSUARENCE OFFICER GRADE II) ZPSI-04: NAFASI 1**

**SIFA ZA MUOMBAJI**

- Awe na elimu ya Shahada ya kwanza ya Sanaa ya Ualimu au ya Sayansi ya Ualimu, Sheria au fani inayolingana nayo kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na uwezo mzuri wa kutumia Kompyuta
- Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea
- Awe na umri usiozidi miaka 40
- Awe Mzanzibari mkaazi

**MAJUKUMU**

- Kuandaa sera,miongozo na kanuni za kudhibiti ubora wa programu na mafunzo ya Sheria kwa vitendo kwa Skuli ya Sheria Zanzibar;
- Kukusanya, kuchambua na kutafsiri mifumo ya Kitaaluma ya Taasisi;
- Kusaidia kufanya mapitio ya mifumo kwa lengo la kudhibiti ubora wenye tija kwa Taasisi;
- Kubaini changamoto zinazokwamisha ubora katika kazi za elimu inayotolewa;
- Kutoa ushauri wa hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika udhibiti wa ubora na viwango kwa maendeleo ya Taasisi.;
- Kusaidia kudhibiti mahudhurio na uwajibikaji kwa wakufunzi kwa lengo la kuimarisha ubora na viwango vya elimu kwa Taasisi.;
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi kwa wakati ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka; na
- Kufanya kazi nyengine zozote kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

**SIFA YA ZIADA**

- Ambae amesomea fani ya Ualimu na Shahada ya Sheria atazingatiwa.

**2. MKUFUNZI MWANDAMIZI WA SHERIA KWA VITENDO (SENIOR LECTURER) ZPSN-01: NAFASI 1**

**SIFA ZA MUOMBAJI**

- Awe na elimu ya Shahada ya Uzamivu ya sheria au inayolingana nayo kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
  au
- Awe na Shahada ya Uzamili ya sheria na uzoefu wa kazi za kisheria
- Awe na uwezo mzuri wa kutumia Kompyuta;
- Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea;
- Awe na umri usiozidi miaka 40;
- Awe Mzanzibari mkaazi.

**SIFA YA ZIADA**

Awe na uzoefu wa kufanya kazi za uwakili.

**MAJUKUMU**

- Kutoa mafunzo ya Sheria kwa vitendo kwa wanafunzi wa Skuli ya Sheria Zanzibar;
- Kutayarisha vifaa vya kusomea na mafunzo ya mazoezi kwa wanafunzi;
- Kuwaongoza na kuwasimamia wanafunzi katika kuwajengea uwezo wa kutayarisha tafiti;
- Kutunga mitihani ya Skuli ya Sheria;
- Kufanya kazi za tafiti na machapisho ya Skuli ya Sheria;
- Kupitia na kutoa mapendekezo ya Mitaala ya Skuli ya Sheria Zanzibar;
- Kuandaa miongozo na sera kwa ajili ya kuboresha Taaluma inayotolewa na Skuli ya Sheria Zanzibar;
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka; na
- Kufanya kazi nyengine zozote kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

**3. MKUFUNZI MSAIDIZI WA SHERIA KWA VITENDO**

**DARAJA LA II (ZPSI-07): NAFASI 2**

**SIFA ZA MUOMBAJI**

- Awe na elimu ya Shahada ya Sheria katika fani ya Sheria kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, uzoefu katika kazi za kisheria unazingatiwa.
- Awe na uwezo mzuri wa kutumia Kompyuta;

- ❖ Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea;
- ❖ Awe na umri usiozidi miaka 40;
- ❖ Awe Mzanzibari mkaazi.

**MAJUKUMU**

- ❖ Kufundisha wanafunzi wa Sheria kwa Vitendo;
- ❖ Kusaidia kusimamia wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo ambao wapo kwenye usimamizi maalumu;
- ❖ Kusaidia kuratibu kazi za ufundishaji kwa wahadhiri wa muda wa ziada na kusimamia ufundishaji;
- ❖ Kutayarisha nyenzo na maudhui ya kusomea wanafunzi;
- ❖ Kutoa ushauri na huduma za semina za Taasisi;
- ❖ Kuandaa mitihani, kusahihisha na kuweka matokeo kwa mujibu wa taratibu;
- ❖ Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka; na
- ❖ Kufanya kazi nyengine zozote kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

**JINSI YA KUOMBA**

Barua za maombi zielekezwe kwa:

Mkuu wa Skuli
Skuli ya Sheria Zanzibar
S.L.P 1418
Michenzani (Michenzani
Mall)
Zanzibar.

Barua ziambatanishwe na taarifa binafsi ya muombaji (CV) yenye picha ya "passport size" iliyopigwa karibuni. Vivuli vya Cheti cha kuzaliwa, Kitambulisho cha Mzanzibar mkaazi na vyeti vya kumalizia masomo. Maombi yote yafanyike kupitia

Mfumo wa ZanAjira (www.portal.zanajira.go.tz). Mwisho wa kupokea maombii hayo **umesogezwa hadi tarehe 5 Disemba, 2023**. Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Skuli ya Sheria Zanzibar www.lsz.ac.tz

**Tanbihi:**

Waombaji wote waliosoma nje ya Nchi ya Tanzania wanatakiwa kuwasilisha cheti cha Uthibitisho kutoka Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Kwa Mawasiliano zaidi wasiliana na namba hizi 0774884889 / 0773076805

**AHSANTENI**